

## **Amri ya Nane ya Mungu: Makatazo na Amri**

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · December 19, 2016

Mafundisho ya Katekismu · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Amri za Mungu

Amri ya Nane ya Mungu inatukataza nini?

Inakataza haya:

1. Ushahidi wa uongo, kiapo cha uongo na uongo wowote. 2. Hukumu isiyo ya haki, usengenyaji, uchafuzi wa jina na usingiziaji. 3. Kusifu watu uongo, kujisifu mwenyewe au ulaghai.

Katika Amri ya Nane Mungu anaamuru nini?

Katika Amri ya Nane Mungu anaamuru tuseme ukweli na tulinde heshima ya wengine. (Mt 5:37, Yak 5:12).

Twaharibu heshima ya wengine kwa namna gani?

Twaharibu Kwa

1. Kuwadhania vibaya 2. Kuwasenganya (Mith 12:22) 3. Kuwasingizia na kuleta uzushi. (Mdo 5:1-11; Law 19:11)

Aliyeharibu heshima ya mwingine yampasa afanye nini?

Aliyeharibu heshima ya mwingine yampasa kuirudisha kadiri awezavyo.

Tunalinda heshima ya wengine kwa namna gani?

Tunalinda heshima ya wengine kwa kuwaza na kusema mema juu yao. (1Kor 13:6)